



Chapisho la ekari

Mapendekezo ya Kilimo mchanganyiko cha muhogo na viazi vitamu Tanzania



HATUA 1: Amua kama kilimo mchanganyiko kina faida zaidi

Kilimo mchanganyiko kitapunguza mavuno ya muhogo kwa makadirio ya asilimia 20 na asilimia 40 kwa viazi vitamu ukilinganisha na kilimo cha zao moja.

Kilimo cha mazao mchanganyiko kitakuwa na faida zaidi iwapo thamani ya viazi vitamu vilivyochanganywa na muhogo itazidi thamani ya mavuno ya muhogo yaliyopungua kutokana na kilimo mchanganyiko.

Tumia jedwali kutathimini kama kilimo mchanganyiko kina faida kwa Kuzingatia Matarajio ya bei ya muhogo na viazi vitamu.

- Kilimo mchanganyiko cha muhogo na viazi vitamu kitapunguza mapato. Panda muhogo peke yake .
- Kilimo mchanganyiko cha muhogo na viazi vitamu kitaongeza mapato kwa kiasi. Panda kwa mchanganyiko kama unataka mapato ya haraka kutoka kweye viazi vitamu.
- Kilimo mchanganyiko cha muhogo na viazi vitamu kitaongeza mapato kwa kiwango kikubwa . Panda kwa kuchanganya muhogo na viazi vitamu.
- Kilimo cha viazi vitamu bila kuchanganya na muhogo kina mapato makubwa. Panda viazi vitamu peke yake.

Bei ya zao la viazi vitamu (TZS / kg)

	100	200	300	400	500	600	700	800	900	1000
100	Green	Green	Green	Black	Black	Black	Black	Black	Black	Black
200	Orange	Green	Green	Green	Green	Black	Black	Black	Black	Black
300	Orange	Orange	Green	Green	Green	Green	Green	Green	Green	Black
400	Orange	Orange	Orange	Green	Green	Green	Green	Green	Green	Green
500	Orange	Orange	Orange	Orange	Green	Green	Green	Green	Green	Green
600	Orange	Orange	Orange	Orange	Orange	Green	Green	Green	Green	Green
700	Orange	Orange	Orange	Orange	Orange	Orange	Green	Green	Green	Green
800	Orange	Orange	Orange	Orange	Orange	Orange	Orange	Green	Green	Green
900	Orange	Orange	Orange	Orange	Orange	Orange	Orange	Orange	Green	Green
1000	Orange	Orange	Orange	Orange	Orange	Orange	Orange	Orange	Orange	Green

HATUA 2: Chagua mbegu sahihi na mpangilio bora wa upandaji

Iwapo umeamua Kulima kilimo mchanganyiko cha muhogo na viazi vitamu panda kama ifuatavyo:

Panda mbegu bora kama Kizimbani, Mahonda au Machui. Tunapendekeza kutumia vipando visivyokuwa na magonjwa kutoka kwenye vyanzo vilivyothibitishwa ili kuhakikisha zao la muhogo ni safi na lenye afya. Panda muhogo kwenye mstari ndani ya matuta yaliyoachana kwa mita 1 na acha nafasi ya mita 1 kati ya vipando vya muhogo (panda vipando 4,000 vya muhogo kwa ekari).

Panda mbegu ya viazi vitamu iliyoreshwa kama Mayai, Kabodea au Mataya. Tunapendekeza utumie vipando safi kutoka kwenye mimea yenye afya ili kudhibiti maambukizi ya fukusi wa viazi na kuzuia kusambaa kwa magonjwa. Siku hiyo hiyo baada ya kupanda muhogo, panda viazi vitamu kipando kimoja cha kiasi kitamu Katikati ya kila vipando viwili vya muhogo (panda vipando 4,000 vya viazi vitamu kwa ekari).

Zingatia, matumizi ya mbolea za viwandani ili kuongeza mavuno na faida (angalia ukurasa wa nyuma).